JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Kingalu
S.L.P 845,
67109 MOROGORO
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MOROGORO APRILI 28, 2020.

MAAFISA WA UMMA WAKATAA KUPOKEA HONGO

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwanza niwashukuru kwa kuitikia wito wetu ili niweze kuzungumza nanyi kwa ajili ya kuuhabarisha Umma juu ya utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoa wa Morogoro.

Ndugu wandishi wa Habari

Kwa hivi karibuni vimejitokeza vitendo vinavyofanywa na wananchi vya kuwashawishi kutaka kuwapa hongo maafisa wa umma wanapotekeleza majukumu yao.

Kwa kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020 tumewakamata na kuwafikisha mahakamani wananchi wawili kwa vipindi tofauti kwa kutaka kuwahongo maafisa wa TAKUKURU na Jeshi la POLISI wakati wakitekeleza majukumu yako.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Misenge kilichopo kata ya Doma Wilayani Mvomero alijaribu kumhonga Afisa wa TAKUKURU kiasi cha Shilingi 200,000/= ili asiweze kumleta mtuhumiwa aliyekuwa anatafutwa na TAKUKURU.

Vile vile Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kipolisi Luhembe alikataa kuhongwa kiasi cha Shilingi 340,000/= toka kwa mtuhumuwa ili awasaidie na kuwaachia baada ya kukutwa na biashara haramu ya madawa ya kulevya.

Kama mjuavyo kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa wananchi kuhusu watumishi wa umma wasiokuwa waadilifu ambao wamekuwa wakiomba rushwa wakati wanapotekeleza majukumu yao.

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro tumeweza kufuatilia na hatimaye kuwakamata na kuwafikisha mahakamani watumishi waliokuwa wakiomba rushwa wakati wanatekeleza majukumu yao kama ifutavyo:

- Askari watano wa Hifadhi ya Taifa (TANAPA) iliyopo hifadhi ya Taifa Mikumi Mkoani Morogoro waliomba na kupokea hongo kiasi cha sh 2,040,000/= toka kwa majangili waliowakamata wakiwa ndani ya hifadhi na walipopatiwa fedha hizo waliachia bila kufuata utaratibu.
- Askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) pamoja n askari wa Jeshi la Akiba (mgambo) waliomba na hongo ya kiasi cha sh 2,000,000/= na kupokea kiasi cha sh 600,000/= toka kwa wakulima waliokutwa wakifanya shughuli za kilimo katika bonde la Mto Kilombero.
- Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji aliomba na kupokea hongo ya kiasi cha sh 30,000/= toka kwa mfanyabiashara ili asimchukulie hatua kwa kutokuwa na cheti cha usalama wa majanga ya moto (***Fire Safety Certificate***).
- Vile vile Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mikumi iliyoko Wilayani Kilosa aliomba shilingi 400,000/= na kupokea hongo ya kiasi cha sh 100,000 toka kwa Daktari Hospitali ya St Harry ili aweze kumuondolea kesi iliyokuwa akiisikiliza.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Aidha katika sekta ya Ardhi imekuwa ikilalamikiwa na wananchi kuhusu vitendo vya rushwa kushamiri katika upatikanaji wa huduma mbalimbali. Kwa kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020 TAKUKURU mkoa wa Morogoro tumeweza kurejesha kiasi cha Shilingi Milioni Mbili na Laki Tatu na Elfu Sitini (**shs 2,360,000/-**) kwa wananchi zaidi ya kumi na watano (15) wa Wilaya ya Kilosa ambao walitapeliwa na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mlimani Boma kilichopo Kata ya Kasiki Wilaya ya Kilosa **- Hosea Nicodemas Mgunda** kwa madai kwamba atawapimia viwanja katika eneo la Mlimani Boma huku akijua eneo hilo limehifadhiwa na Serikali kwa matumizi ya shughuli za Umma.

Vile vile TAKUKURU imeweza kurejesha kiasi cha **Shilingi Millioni tatu na laki nne (sh. 3,400,000/=)** kwa wananchi wa Wilaya ya Mvomero ambao walitozwa na mwenyekiti wa kijiji, Mtendaji wa Kata na Afisa Ugani wa Mlali kwa kukiuka maelekezo yaliyotolewa na Baraza la Maendeleo ya Kata kwa kuamuru kuuza maeneo kwa wananchi kinyume na utaratibu

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Mwezi Januari 2020 **hadi Machi 2020**, tulipokea jumla ya taarifa **132** ambapo tumeweza kufungua kesi mpya nane na kati ya hizo kesi tumeweza kushinda kesi tatu.

Ndugu wandishi wa Habari

UZUIAJI RUSHWA

Katika kudhibiti vitendo vya rushwa, Tumeweza kuokoa kiasi cha cha **shilingi Milioni Hamsini na Saba Mia Nane na Sabini na Tisa Elfu Mia Saba Ishirini na Tano (sh 57,879,725/=)** ambazo zilikuwa mikononi kwa viongozi wa vyama vya Ushirika na SACCOS katika Wilaya za Mvomero na Gairo. Watuhumiwa wanaendelea kurejesha fedha ambazo walizifanyia ubadhirifu kinyume na malengo ya vyama hivyo.

Pia TAKUKURU ilibaini kuwepo kwa wateja sugu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro kutokulipa madeni yao yaliyotokana huduma ya Majitaka. Katika ufuatiliaji huo Mamlaka imeendelea kulipwa fedha toka kwa wateja hao. Aidha katika kudhibiti ubadhirifu huo Mamlaka imelipwa kiasi cha sh 3,000,000/= kati ya shs 13,386,932.40 zinazodaiwa kwa wateja waliotumia huduma hiyo.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika uelimishaji Umma TAKUKURU imekuwa ikitoa mafunzo ya rushwa na madhara yake ambapo kwa kipindi cha mwezi **Januari 2020** hadi **Machi 2020**, **tulifungua na kuimarisha klabu za wapinga rushwa zipatazo Mia Moja na Ishirini na Tatu (123)** katika shule za msingi, sekondari na vyuo, kufanyika kwa **mikutano hadhara na mijadala ya wazi Arobaini na Mbili (42),** kuendesha mafunzo na **semina Kumi na Moja (11)** kwa makundi mbalimbali, tulirusha **vipindi vya redio na tv Vitano (5) na tuliandaa Makala Kumi na Nane (18)** na **utoaji wa habari kwa umma (1)**.

Ndugu Waandishi wa Habari

UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Kwa kipindi cha Mwezi Januari 2020 hadi Machi 2020 tuliendelea kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika Mkoa Morogoro. Katika ufuatiliaji huo tumeweza kubaini kuwepo kwa ukiukwaji wa masharti ya vipengele vya Mkataba ulioingiwa kati ya Halmashauri ya Wilaya Malinyi pamoja na Kampuni ya Ujenzi iitwayo Deep Construction Ltd kwa gharama ya kiasi cha sh 225,061,990 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi na kiasi cha sh 123,273,499.9 kwa ajili ya ujenzi wa Dampo.

Aidha katika ufuatiliaji huo TAKUKURU imeweza kuishauri Halmashauri hatua za kuchukua dhidi ya Mkandarasi na kwamba mnamo tarehe 15/03/2020 Halmashauri hiyo iliweza kuvunja mkataba na mkandarasi huyo.

Ndugu Waandishi wa Habari

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Kamati za Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya kwa kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhi ya rushwa katika Mkoa wetu.

Ndugu Waandishi wa Habari

TAKUKURU inatoa wito kwa Halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro zilizopokea michango na misaada kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa COVID 19 ziweze kutumika kwa lengo la kupambana na Corona kama ilivyokusudiwa.

Aidha TAKUKURU haitasita kuwachukulia hatua wote watakaohujumu mapambano na kujikinga na CORONA.

Vilevile tunawasihi wananchi waendelee kuunga mkono jitihada zinazofanywa na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa.

Imetolewa na:

Victor Swella
Naibu Mkuu wa TAKUKURU,
Morogoro